

Wiki ya Kuchukua Hatua ya Maisha ya Watu Weusi ni Muhimu katika Shule za DeKalb

Kuadhimisha Michango ya Watu Weusi Marekani - Kongamano la Mtandaoni la Moja kwa Moja

Vikao Sambamba vya Kongamano la Mtandaoni:

- Chagua kikao kimoja kwa kila kifaa.
- Bofya kwenye mada ya bluu ili ujunge na kikao saa 11:00am.

Tumeratibu wazungumzaji na mada mahiri ili uweze kujihusisha na kujifunza zaidi kuhusu matokeo ambayo Waafrika Wamarekani wameleta nchini Marekani. Kwa wakati uliowekwa, wakati wa kongamano la mtandaoni utaombwa ubofye kiungo katika kipengele cha gumzo.

Kikao cha 1: Mizizi ya Kina: Historia na Urithi wa Waafrika Wamarekani

Mzungunzaji: Mawuli Davis

Waafrika Wamarekani wamechangia ustawi wa Kaunti ya DeKalb na kote ulimwenguni. Utajifunza kuhusu viongozi Waafrika Wamarekani ambao walishawishi na kuunda nchi na vitongoji vyetu tunavyoishi leo, na maendeleo yaliyofanywa kwa miaka mingi katika serikali, elimu, biashara na mashirika ya jamii.

Kikao cha 2: Watu Weusi na STE(A)M

Mzungumzaji: Dak. Noreen Khan-Mayberry

Watu weusi wametoa mchango muhimu katika nyanja ya STE(A)M inayounda ulimwengu wetu, na tunahitaji watu zaidi kama hawa. Uwiano wa shahada za kwanza katika sayansi zilizotunukiwa wahitimu Watu Weusi ulisalia pale pale kwa takriban asilimia 9 kutoka 2001 hadi 2016, kulingana na takwimu zinazopatikana hivi karibuni zaidi kutoka Shirika la Kitaifa la Sayansi; katika uhandisi, ulipungua kutoka asilimia 5 hadi asilimia 4; na katika hesabu, ulishuka kutoka asilimia 7 hadi asilimia 4. Katika kipindi hiki, wanafunzi watakutana na kujifunza kuhusu watu weusi wengi wanaovutia ambao ni waundaji, watayarishi na wabunifu katika STE(A)M.

Kikao cha 3: Ni Sawa Kuomba Usaidizi: Ustawi wa Akili katika Jamii za Watu Weusi

Mzungunzaji: Dak. Nicole Prad Jennings

Marekani ina 13.4% ya wakazi wake wanaojitambua kama Watu Weusi au Waafrika Wamarekani na kati ya hao, zaidi ya 16% waliripoti kuwa na matatizo ya akili, hiyo ni takriban watu milioni 7. Kulingana na utafiti wa hivi majuzi kutoka kwa Mental Health of America, licha ya viwango hivi kuwa chini ya idadi ya jumla ya watu wa Marekani, matukio makubwa ya mfadhaiko yaliongezeka kutoka asilimia 9 hadi asilimia 10.3 kwa vijana Weusi na Waafrika Wamarekani wenye umri wa miaka 12-17, asilimia 6.1 hadi asilimia 9.4 kwa vijana wadogo wa 18-25, na asilimia 5.7 hadi asilimia 6.3 katika kundi la umri wa miaka 26-49 kati ya 2015 na 2018.

Kikao cha 4: Hadithi za Watoto Weusi

Wazungumzaji: Hootdini na Bw.Cobb

Wafrika-Wamarekani wameandika vitabu vingi ambavyo vimepitishwa kutoka kizazi kimoja hadi kingine. Hootdini na Bw. Cobb wetu watasimulia tena vitabu vya watoto vya waandishi maarufu wa asili ya Waafrika Wamarekani.

Kikao cha 5: Usawa wa Utajiri katika Jamii ya Watu Weusi

Mzungunzaji: Royce Richardson

Kuziba pengo la utajiri wa kati ya wazungu na watu wa rangi kunahitaji uinujaji mkubwa na kuwaza kimaendeleo. Kulingana na Taasisi ya Brookings, kaya ya wastani ya wazungu ina thamani mara 10 ikilinganishwa kaya wastani ya Watu Weusi. Ikiwa kaya za Watu Weusi zingekuwa na sehemu ya utajiri wa kitaifa kulingana na sehemu yao ya idadi ya watu wa Marekani, ingekuwa dola trilioni 12.68 katika utajiri wa kaya, badala ya jumla halisi ya dola trilioni 2.54. Pengo la jumla la utajiri kati ya wazungu na watu wa rangi, kwa hivyo, ni dola trilioni 10.14. Katika kikao hiki, utasikia kutoka kwa wataalamu kuhusu jinsi tunavyoweza kuziba pengo la utajiri kati ya wazungu na watu wa rangi.

Kikao cha 6: Kwa Watu, kutoka kwa Watu: Mifumo Isiyo na Usawa wa Mahakama na Sheria

Mzungumzaji: Kayla Kudratt

Kuna utofauti kati ya wazungu wa watu wa rangi katika Mfumo wa Haki wa Marekani. Kulingana na ripoti ya hivi majuzi ya The Sentencing Project, mwaka wa 2016, Wamarekani weusi walijumuisha 27% ya watu wote waliokamatwa nchini Marekani—mara mbili ya sehemu yao ya jumla ya watu wote. Vijana weusi wanajumuisha 15% ya watoto wote katika Marekani lakini walijumuisha 35% ya watoto waliokamatwa katika mwaka huo. Katika kikao hiki, utajifunza kuhusu mifumo isiyo na usawa na jinsi tunaweza kuvunja desturi hii.